Kioo cha Lugha, Juz. 24(1), 71-83
Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam DOI: https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v24i1.5

Uchambuzi wa Ufupishaji wa Majina WanayopewaWasukuma Nchini Tanzania

Winifrida Moshi[1], *Zelda Elisifa*[2], *Jacob Leopold*[3]

Ikisiri

Utafiti huu umechambua ufupishaji wa majina wanayopewa Wasukuma kwa kuchunguza namna ufupishaji huo unavyofanyika baina yao wakati wa mawasiliano ya kila siku ili kurahisisha mawasiliano miongoni mwao. Utafiti umechambua majina ya asili ya Kisukuma na majina ya kigeni wanayopewa watoto wanapozaliwa. Uchambuzi wa majina umefanyika kwa kuzingatia dhana ya onomastikia ambayo hushughulikia majina ya mahali na majina ya watu. Utafiti huu umejikita kwenye dhana ya anthroponomastiki kwa kuangalia namna majina ya watu yanavyofupishwa wakati wa mazungumzo ya watu wa jamii za Kisukuma. Utafiti ulifanyikia katika wilaya ya Sengerema, mkoani Mwanza, ukiongozwa na Nadharia ya Uchanganuzi Tahakiki Usemi. Utafiti ulihusisha jumla ya wazee wazawa 20 waliopatikana kutoka kwenye vikundi viwili vya kahawa na wanafunzi kutoka shule ya msingi Bugalama na shule ya msingi Katunguuru. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa, majina wanayopewa Wasukuma hufupishwa mwanzoni, mwishoni, katikati au kutumia majina ambatani ili kurahisisha mawasiliano miongoni mwa jamii hiyo. Mapendekezo yanatolewa kwa watafiti wengine kuchunguza na kuchambua namna ufupishaji wa majina ya watu unavyofanyika kwa jamii zingine kwa kuangalia majina ya asili na majina ya kigeni.

1.0 Utangulizi

Kila kiumbe na hali hupewa majina na binadamu ili kurahisisha mawasiliano na kusaidia katika utambuzi wa haraka wa kinachozungumziwa. Massamba (2004) anaeleza kuwa jina ni neno linalotumika kutaja vitu (mfano kiti, meza, na chungu), kiumbe (mfano mtu, ndege, mnyama au mtu), sehemu (mfano, Mtwara na Tabora), tendo-jina (mfano kusukuma na uainishaji) na hali (mfano majonzi na furaha). Wanaisimu mbalimbali wanadokeza kuwa neno linalotumiwa kutaja kiumbe au hali

[1] Mkufunzi Msaidizi, Idara ya Mafunzo, Taasisi ya Elimu ya Watu wazima, Tanzania. Barua pepe: winifrida.moshi@iae.ac.tz
[2] Mhadhiri Mwandamizi, Idara ya Isimu, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Tanzania. Barua pepe: zelda.elisifa@out.ac.tz
[3] Mhadhiri Mwandamizi, Idara ya Isimu, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Tanzania. Barua pepe: jacob.leopold@out.ac.tz

aghalabu huchukuliwa kiisimu kama nomino. Hivyo basi, nomino ni neno linalotumiwa kutaja jina la mahali, mtu, kitu, hali au hata kitendo (TUKI, 2004). Licha ya kuwa kuna aina nyingi za nomino, utafiti huu ulijikita katika kuchambua ufupishaji wa majina ya watu yanayotumiwa na jamii za Kisukuma katika wilaya ya Sengerema.

Onomastiki ni aina ya taaluma inayochunguza majina ya viumbe (Crystal, 1987). Taaluma hii inajumuisha mbinu za kutambulisha majina ya watu na mahali. Majina ya watu yanaweza kurejelewa kama anthroponemia. Kwa upande mwingine, stadi za majina ya mahali hurejelewa kama toponomastiki ambayo hufupishwa kama toponimia/toponemia. Hivyo basi, taaluma ya onomastiki inagawika katika makundi mawili: anthroponomastiki, yaani taaluma inayorejelea majina ya binadamu na toponomastiki ikiwa ni taaluma inayohusiana na majina ya mahali. Utafiti huu uliangazia taaluma ya anthroponomastiki.

1.1 Lugha ya Kisukuma

Mekacha (2011) anaeleza kuwa Kisukuma ni lugha mojawapo kati ya lugha za Kibantu zinazopatikana nchini Tanzania. Lugha hii huzungumzwa katika mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Tabora, Geita na Simiyu. Wasukuma wanajishughulisha na shughuli za uzalishaji mali kama vile kilimo cha mahindi, pamba, mpunga, mtama na alizeti pamoja na ufugaji wa ng'ombe, mbuzi na kondoo. Kisukuma kinatumiwa na watu wengi lakini kinapambana na changamoto ya kuingiliwa na matumizi ya lugha ya Kiswahili. Kama watumiaji wataendelea kukitumia nyumbani na kukiandika, kitaendelea kuishi kwa vizazi vijavyo.

1.2 Dhana ya Anthroponomastiki

Aina hii ya onomastikia hutumiwa kurejelea majina ya binadamu. Kwa mujibu wa Msanjila, Kihore na Massamba (2009), anthroponomastiki ni tawi la onomastiki linalohusika na uchunguzi wa majina ya watu, asili yake na maana yake na jinsi yanavyotumika katika jamii fulani. Wataalamu hawa wamegawanya uchunguzi wa anthroponomastiki kwa kuangalia asili ya jina, maana, aina za majina na matumizi ya kijamii ya jina. Kwa ujumla, wataalamu hawa wanaliona jina kama hati ya utambulisho wa kijamii na kiutamaduni.

Muzare (2000) anasema majina ya Kiafrika huwa na kazi nyingi. Kila jina ni ujumbe, historia na sala kutoka kwa wazazi. Tofauti na majina ya Magharibi, majina ya Kiafrika hayatolewi kiholela, yana dhamira. Wakati mwingine majina hayo huonesha kumbukumbu ya matukio makubwa yaliyotokea katika jamii, au kuelezea maumbile, mwonekano, tabia au sifa za mtoto aliyezaliwa. Naye Mutembei (2009) anaeleza suala la majina kwa kujikita katika majina ambayo yaliibuka baada ya kuja kwa ugonjwa wa UKIMWI. Maswali anayojiuliza ni kwamba, 'sababu zipi ziliwafanya watu kutoa majina katika vitu, hali au tukio?' 'Je, majina hayo yalikuwa na maana gani?' 'Je, majina hayo yalikuwa kielelezo kwa yale yaliyotokea?' Mtaalamu huyu anatoa majibu na anaeleza kwamba majina

yaliyotolewa kimsingi yalikuwa na msukumo ambao uliwafanya wayatoe majina hayo. Katika utafiti huu, mtafiti alichambua majina wanayopewa Wasukuma nchini Tanzania na namna ufupishaji wa majina hayo unavyofanyika.

1.3 Mapitio ya Kazi Tangulizi

Adams (1973) anaeleza kuwa ufupishaji wa majina ni mchakato wa kuondoa silabi moja au mbili katika majina bila kusababisha mabadiliko yoyote ya kimaana katika matumizi yake. Otlogestswe na wenzake (2022) katika makala yao ya uundaji wa majina ya utani kwa kutumia njia ya ufupishaji wa majina, wanaeleza kuwa majina hufupishwa kwa lengo la kuelezea tabia ya mtu, kutoa maoni ya maisha ya mtu kwa familia au jamii inayomzunguka, kukumbuka tukio la muhimu lililotokea wakati anaitwa jina hilo na kurahisisha utambuzi wa jina hilo kwa mhusika wa jina. Bauer (1983) anasema kuwa hakuna njia mahususi ya kujua kuwa ni maneno mangapi hukatwa wakati wa ufupishaji kwa kuwa ufupishaji unaweza kufanyika katika sehemu yoyote ya jina. Kwa hiyo, ufupishaji wa majina ni uondoaji wa baadhi ya silabi kwenye jina ili kurahisisha mawasiliano miongoni mwa wazungumzaji wa lugha husika. Utafiti huu ulijikita kwenye ufupishaji wa majina wanayopewa Wasukuma, yakiwamo majina ya asili ya Kisukuma na majina ya kigeni.

Marchand (1969) anaeleza kuwa ufupishaji ni mchakato wa kuunda neno jipya kwa kupunguza sehemu za neno refu, bila kubadili maana ya msingi. Anaendelea kusema kuwa neno linalofupishwa linaendelea kuwa ni aina ileile ya neno na maana haibadiliki. Mara nyingi ufupishaji hufanyika ili kuonesha ukaribu au urafiki wa wazungumzaji au watumiaji wa lugha. Rico-Sulayes (2020) alichunguza majina ya utani yanayotokana na ufupishaji wa majina halisi ya watu. Uchunguzi wake ulijikita katika matumizi ya irabu ‘I’ ambayo huongezwa kwenye ufupishaji au jina la utani. Hata hivyo, matokeo ya uchunguzi wake yalionesha kuwa ufupishaji huo hauhusiani na masula ya kijinsia isipokuwa ni mazoea tu miongoni mwa watumiaji.

Newman na Mustapha (1992) walichunguza majina ya utani katika lugha ya Kihausa. Katika utafiti wao walibaini kwamba majina ya utani hutokana na miundo ya urudufishaji wa sauti, hususani kiambishi tamati. Adams (1973) anaeleza kuwa ufupisahaji mara nyingi hutokea katika majina ambapo silabi moja au mbili huondolewa kwenye neno na maana haibadiliki. Bauer (1983) anafananisha mawazo yake na Adams kwa kueleza kuwa ufupishaji ni mchakato wa uundaji wa maneno ambapo sehemu moja au zaidi ya neno refu hufutwa ili kubaki na sehemu fupi inayoweza kusimama yenyewe na kuwa na maana ileile. Anasisitiza kuwa ufupishaji hutumiwa zaidi kwenye mazungumzo, magazeti ya michezo na lugha ya vijana; ufupishaji hautumiki sana kwenye maandishi rasmi ya kisheria. Mattiello (2013) anaeleza kuwa kukata neno/maneno ni mchakato wa kufupisha neno kutokana na utamkaji au uandishi na maana sahihi ya neno hilo hupotea kwa kuwa ni sehemu tu ya neno inayobaki na si neno zima.

Marchand (1969), López-Rúa (2002), Plag (2003), Fandrych (2004) na Mattiello (2013) wamechambua na kujadili mgawanyo wa ukataji wa majina ya watu kwa kuyaweka katika makundi matano. Makundi haya yanawasaidia watafii kuangazia ni makundi yapi ya ukataji yanapatikana katika majina ya asili na yale ya kigeni wanayopewa watoto wa jamii ya Kisukuma wanapozaliwa:

i) Ufupishaji wa majina ya watu mwishoni mwa jina: ufupishaji huu huondoa baadhi ya viambishi vya jina na kulifanya jina hilo kuwa fupi kulingana na matakwa ya mtakaji na namna anavyofikiria inaweza kueleweka kwa mwenye jina au kwa mtu anayesikiliza. Mfano wa jina linaweza kuwa *Juliana* na kufupishwa kwa kuondolewa viambishi mwishoni mwa jina hilo na kuwa *Juli*. Hapo silabi mwishoni mwa jina zimeondolewa kutoka *Juliana* na kuwa *Juli.*

ii) Ufupishaji majina mwanzoni mwa jina: ufupishaji huu huondoaa viambishi mwanzoni mwa jina na kufanya jina kuwa fupi na linaloeleweka kwa mwenye jina na msikilizaji. Mfano jina *Christina,* linaweza kufupishwa kwa kuondolewa silabi mwanzoni na kuwa *Tina*.

iii) Ufupishaji wa majina kwa kuondoa viambishi katikati ya jina: viambishi huondolewa katikati ya jina na kufanya jina kuwa fupi na lenye kueleweka kwa mwenye jina au msikilizaji. Mfano wa jina linaloondolewa viambishi katikati ni *Nh'olombi*. Jina hili huweza kuondolewa viambishi katikati ya jina na kuwa *Nh'ombi*. Kiambishi 'lo' kimeondolewa katika jina.

iv) Ufupishaji wa majina katika sehemu ya neno lililoungana au jina ambatani na kuwa jina moja: ukataji huu hufanyika kwenye yale majina ambatani. Mfano *Yelamayanda;* jina hili linaweza kukatwa na kuwa *Yela* au *Mayanda*.

v) Ufupishaji wa jina kwa kufuta vipenegele vya neno ambapo kiambishi tamati huongezwa baadaye. Aina hii ya ukataji hutokea zaidi kwenye majina ya Kijapani. Ufuatao ni mfano wa majina ya Kijapani:

Jina	**Ufupisho**	**Ongeza –"chan"**	**Jina Linalotokea**
Katsuki	*Katsu*	*Katsu-chan*	*Katchan*
Uchimura	*Uchi*	*Uchi-chan*	*Utchan*

Tafiti ambazo zimefanywa na wataalamu hao zimeacha pengo la uchambuzi wa ufupishaji wa majina ya watu wanayopewa Wasukuma wanapozaliwa.

2.0 Misingi ya Nadharia na Methodolojia

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Uchanganuzi Tahakiki Usemi (UTU). Nadharia hii iliasisiwa na Norman Fairclough mwaka 1989 na hushughulikia masuala ya lugha na utamaduni wa jamii. Pia, nadharia hii inachunguza miktadha ya kijamii kwa kutazama lugha kama uzoefu wa wanajamii. Uchanganuzi wa usemi hudhihirisha michakato mitatu ya muktadha. Mchakato wa kwanza ni wa muktadha wa kihistoria ambayo hujumuisha matukio yanayotokea katika jamii hiyo.

Muktadha wa pili ni wa kiutamaduni ambao unaelezea kwa kujua mila na desturi, imani na maadili ya jamii husika. Muktadha wa tatu ni wa hali ambayo huonesha kuwa lugha hubadilika kulingana na mahali, wakati na watu walipo, na lengo la mazungumzo. Utafiti huu umetumia mchakato wa tatu wa muktadha ambao huchunguza jamii kwa kuzingatia hali ambayo huonesha kuwa lugha hubadilika kulingana na mahali, wakati uliopo, na lengo la mazungumzo. Muktadha huu utasaidia kuonesha namna ambavyo ufupishaji wa majina ya watu unafanywa na Wasukuma katika mazungumzo yao na namna ufupishaji uanavyofanyika

Utafiti huu ulitumia mbinu ya kimaelezo. Utafiti wa kimaelezo ni kupanga, kutoa sababu na kuzieleza data kama zilivyoelezwa na walengwa wa utafiti (Cohen, 2000). Utafiti huu ulihusisha jumla ya watoataarifa 50 ikiwa na jumla ya wazee 20 waliopatikana kutoka kwenye vikundi viwili vya kahawa, yaani kikundi cha Nyamtelela na kikundi cha Katunguru, na wanafunzi 30 kutoka katika shule ya msingi Bugalama na shule ya msingi Katunguru. Kwa kutumia majadiliano ya vikundi lengwa, wazee hawa 20 waliweza kutaja na kuchambua majina ya watu na namna yanavyofupishwa huku wakiendelea kupata kahawa. Data zilizopatikana kwa njia ya majadiliano ya vikundi lengwa ziliwezesha kupata majina hayo na namna yanavyofupishwa na jamii ya Wasukuma. Data zingine zilipatikana kwa njia ya ushuhudiaji kwa wanafunzi wa shule ya msingi Bugalama na shule ya msingi Katunguru, ambapo watafiti walishuhudia namna majina ya wanafunzi hao yalivyofupishwa wakati wa mazungumzo yao.

Majina wanayoitana wanafunzi wakati wa mazungumzo yao ni ya vifupisho ikilinganishwa na majina waliyoandikishwa kwenye daftari la rejesta. Data zilizokusanywa zilichambuliwa kwa maelezo kwa kuwa utafiti huu unaongozwa na mkabala wa maelezo.

3.0 Matokeo ya Utafiti

Kipengele hiki kinawasilisha na kuchambua matokeo ya data ambazo zilikusanywa kwa njia ya majadiliano ya vikundi lengwa kwa wazee wazawa na kwa njia ya ushuhudiaji kutoka kwa wanafunzi wanaosoma shule ya msingi Bugalama na shule ya msingi Katunguru. Utafiti uliongozwa na Nadharia ya Uchanganuzi Tahakiki Usemi (UTU) na uwasilishaji na uchambuzi wa data ulifanyika kwa njia ya maelezo.

3.1 Ufupishaji wa Majina ya Asili katika Lugha ya Kisukuma

Huu ni ufupishaji unaohusu majina ya asili ya lugha ya Kisukuma. Ufupishaji huu hufanyika ili kurahisisha mawasiliano miongoni mwao. Ufupishaji wa majina ya asili ya lugha ya Kisukuma hufanyika mwanzoni, mwishoni, katikati na udondoshaji wa jina moja katika majina ambatani. Aidha, ufupishaji huu hufanyika katika lugha ya mazungumzo.

3.1.1 Kukata Silabi Mwishoni mwa Jina

Katika majina ya asili yaliyochambuliwa katika utafiti huu, imebainika kuwa wakati wa mazungumzo majina hukatizwa ili kuokoa muda wa utamkaji. Ukataji wa viambishi mwishoni mwa jina hufanyika kwa kuondoa viambishi viavyopatikana mwishoni mwa jina.

Mfano 1

Na	**Jina kamili**	**Jina lililofupishwa**	**Viambishi vilivyoondolewa**
i	Mashaka	Masha	‘ka’
ii	Sunduhaja	Sundu	‘haja’
iii	N’hongojiwa	N’honge	‘jiwa’
iv	Kwiyolecha	Kwiyo	lecha’
v	Lusendamiwa	Lusenda	‘mila’
vi	Maduhu	Madu	‘hu’
vii	Ngolelwa	Ngole	‘lwa’
viii	Shilatu	Shila	‘tu’

Chanzo: Data za Utafiti (2025)

Ufupishaji huu wa majina ya watu kwa kuondoa silabi za mwishoni umeonekana kwa namna tofautitofauti. Kuna baadhi ya majina ambayo yameondolewa silabi moja kama Masha… ambapo silabi ‘ka’ imeondolewa katika jina la *Mashaka; Madu*…. silabi ‘hu’ imeondolewa katika jina la *Maduhu.* Mengine yameondolewa silabi mbili na kuendelea, kwa mfano*, Lusenda…* silabi ‘mi’ *na* ‘la’ zimeondolewa katika jina la *Lusendamila; Kwiyo…* silabi *‘le’* na *‘cha’* zimeondolewa katika jina la *Kwiyolecha* na *Sundu*… silabi ‘ha’ na ‘ja’ zimeondolewa katika jina la *Sunduhaja*. Majina haya yanapofupishwa hakuna kanuni mahususi inayozingatiwa katika ufupishaji huo kwani kila mtu hufupisha kulingana na matakwa yake, ijapokuwa kumekuwapo na mazoea ya kufupisha majina kwa ufupi unaofanana. Katika lugha ya Kisukuma, viambishi huondolewa mwishoni ili kulifanya jina kuwa fupi bila kuzingatia ni silabi ngapi au ipi inaondolewa katika jina.

3.1.2 Ufupishaji wa Kuondoa Viambishi Mwanzoni mwa Jina

Majina ya Kisukuma pia huweza kukatwa viambishi mwanzoni mwa jina, suala linalohusisha uondoaji wa viambishi mwanzoni mwa jina. Ifuatayo ni mifano michache ambayo inadhihirisha ufupishaji wa majina ya Kisukuma kwa kuondoa viambishi mwanzoni mwa jina.

Mfano Na 2

Na	**Jina kamili**	**Jina lililofupishwa**	**Viambishi vilivyoondolewa**
i	Makoye	Koye	‘Ma’

ii	Misoji	Soji	‘Mi’
iii	Mashimba	Shimba	‘ma’
iv	Kwinoja	Noja	‘kwi’
v	Shigolile	Golile	‘shi’
vi	Malemi	Lemi	‘ma’
vii	Ng’ipage	Pagi	Ng’wi
viii	Bacholwa	Cholwa	‘ba’
ix	Lusambaja	Sambaja	‘lu’
x	Magembe	Gembe	‘ma”

Chanzo: Data za Utafiti (2025)

Katika majina yaliyoorodheshwa katika Mfano 2, inadhihirishwa kuwa majina hufupishwa wakati wa mazungumzo kwa kuondoa viambishi mwanzoni na kufanya jina hilo kuwa fupi. Katika utafiti huu, kupitia majina yaliyochunguzwa imebainika kuwa ukataji wa majina ya Kisukuma mwanzoni mwa jina huhusisha uondoaji wa silabi moja tu, kwa mfano, katika jina *Cholwa* silabi ‘ba’ imeondolewa katika jina la *Bacholwa, Gembe* silabi ‘ma’ imeondolewa katika jina *Magembe* na *Pagi* silabi ‘ng’wa’ imeondolewa katika jina *Ng’wipagi.*

3.1.3 Ufupishaji Unaofanyika katikati ya Jina

Ufupishaji wa majina ya Kisukuma huhusisha pia ufupishaji wa majina kwa kuondoa viambishi katikati ya jina kama ambavyo tumeona kwenye aina zingine za ufupishaji. Ufupishaji huu huondoa silabi katikati ya jina na kulifanya kuwa fupi. Utafiti huu umechunguza majina kadhaa na kubaini kuwa kuna baadhi ya majina ya asili ya Kisukuma huondolewa baadhi ya silabi katikati ya jina na kufanya jina kuwa fupi. Majina yaliyopo katika data namba tatu yanadhihirisha kuwapo kwa aina hii ya ufupishaji kwenye majina ya watu yenye asili ya Kisukuma.

Mfano 3

Na	**Jina kamili**	**Jina lililofupishwa**	**Viambishi vilivyoondolewa**
i	Makanila	Kani	*‘ma’*na *‘la’*
ii	Makaolobela	Kolobe	*‘ma’* na *‘la’*
iii	Batikalaho	Tikala	*‘ba’* na *‘ho’*
iv	Bashikaho	Shika	*‘ba’* na *‘ho’*
v	Bayugele	Yuge	*‘ba’* na *‘le’*
vi	Shilangile	Langi	*;shi’* na *‘le’*

Chanzo: Data za Utafiti (2025)

Aina hii ya ufupishaji inahusisha uondoaji wa baadhi ya viambishi katikati ya jina. Data katika Mfano 3 inadhirisha namna ambavyo ufupishaji wa majina yenye asili ya Kisukuma unavyoweza kufanyika hata katikati ya jina. Hii inadhirisha kwamba

watumiaji wa lugha hutumia utaratibu wowote ambao wao wanadhani wakiutumia wanaweza kuelewana miongoni mwa watumiaji wa lugha hiyo. Nadharia ya UTU inaeleza kuwa lugha hutumika kama mazoea ya kijamii, kwa hiyo, hata ufupishaji unaofanywa unatokana na mazoea ya jamii husika kupenda kufupisha majina hayo kwa kuwa hakuna kanuni yoyote inayotawala mchakato huo. Mambo hayo yote hutokea katika tukio husika la mawasiliano kama Bauer anavyoeleza (1983) hakuna njia mahususi ya kujua kuwa ni maneno mangapi hukatwa wakati wa ufupishaji kwa kuwa ufupishaji unaweza kufanyika kwenye sehemu yoyote ya neno.

3.1.4 Ufupishaji wa Jina Ambatani

Kuna majina ya Kisukuma ambayo ni ambatani. Majina haya wakati wa utamkaji huweza kufupishwa na kutajwa kama jina moja. Utafiti huu ulichambua majina machache yaliyotolewa na watafitiwa na kubaini kuwa majina ambatani hufupishwa kwa kuondoa jina mojawapo na kubaki na jina moja kama ilivyo katika Mfano 4 ufuatao:

Mfano 4

Na	**Jina Kamili**	**Jina lililofupishwa**	**Viambishi vilivyoondolewa**
I	Miso+Mado	Mado	*Miso*
ii	Yela+manyanda	Yela	*Mayanda*
Iii	Machimu+kenda	Machimu	*Kenda*
Iv	Masala+Munda	Masala	*Munda*
V	Masala+kulangwa	Kulangwa	*Masala*
Vi	Mpanga+mucho	Mpanga	*Mucho*
vii	Busiga+solwe	Busiga	*Solwe*
viii	Igwa+lemi	Lemi	*Igwa*
ix	Imala+ndagu	Ndagu	*Imala*

Chanzo: Data za Utafiti (2025)

Majina yaliyopo katika Mfano 4 yanadhihirisha kuwa majina amabatani yenye asili ya Kisukuma hufupishwa kwa kuondolewa jina mojawapo mwanzoni au mwishoni mwa jina, mfano "*Yela+Mayanda*" kifupi cha jina hili ni "Mayanda" ambapo jina hili limefupishwa mwishoni na hata likifupishwa mwanzoni pia linaleta maana inayoeleweka "*Yela",*. "*Miso+mado*" kifupi cha jina hili ni "*Mado*" ambapo jina hili limefupishwa mwishoni mwa jina na hata likifupishwa mwanzoni bado linaleta maana '*Miso*" lenye maana ya macho. Kwa hiyo, ufupishaji wa majina ambatani huweza kuwa mwanzoni au mwishoni mwa jina. Utafiti huu umechunguza namna majina ya watu yanavyofupishwa miongoni mwa jamii ya Kisukuma wakati wa mawasiliano yao.

3.2 Ufupishaji wa Majina ya Kigeni Yanayotumika katika Jamii ya Wasukuma

Lugha yoyote duniani hukuza msamiati wake kwa kutohoa/kuchukua maneno kutoka katika lugha nyingine. Lugha ya Kisukuma nayo imechukua majina kutoka katika lugha za kigeni. Majina hayo hutumika kama sehemu ya majina yao. Majina hayo ya kigeni yanahusishwa na majina ya dini za Kiislamu na Kikristo. Majina haya yanapotumika katika uwanja wa lugha ya Kisukuma, wazungumzaji wa lugha hii huyafupisha na kuyafanya kuwa mafupi kadiri wanavyoweza kuyatamka wakati wa mazungumzo. Athari hii ya ufupishaji wa majina hujitokeza zaidi kwenye lugha ya mazungumzo ambapo majina hutajwa kwa kufupishwa. Ufupishaji wa majina ya kigeni unahusisha makundi manne ambayo ni ufupishaji mwishoni mwa jina, ufupishaji mwanzoni mwa jina, ufupishaji wa majina katikati ya jina na ufupishaji wa majina ambatani.

3.2.1 Kufupisha Viambishi Mwishoni mwa Jina

Ufupishaji wa majina ya kigeni mwishoni huhusisha uondoaji wa baadhi ya silabi mwishoni mwa jina na kufanya jina kuwa fupi. Kwa kuwa jamii ya Wasukuma ina mazoea ya kufupisha majina hasa katika mazungumzo yake ya kila siku ambapo hulazimika kufupisha hata majina ambayo si ya asili ya lugha ya Kisukuma. Majina ya kigeni ambayo yamefupishwa kwa kuondolewa viambishi mwishoni mwa jina yanadhihirishwa katika Mfano Na. 5 ufuatao.

Mfano 5

Na.	**Jina kamili**	**Jina lililofupishwa**	**Viambishi vilivyoondolewa**
i	Juliana	Juli	‘ana’
ii	Emmanuel	Emma	‘nuel’
iii	Velonica	Velo	‘nica’
iv	Justina	Jusi	‘tina’
v	Marko	Mari	‘ko’
vi	Leonard	Leo	‘nard’
vii	Christopha	Kili	‘stopha’
viii	Debola	Debo	‘ra’
ix	Selemani	Sele	‘mani’

Chanzo: Data za Utafiti (2025)

Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa Wasukuma hufupisha majina ya kigeni wanayopewa wanajamii hao. Watumiaji wa lugha hii hufupisha majina kwa kutamka katika lafudhi yao. Kwa mfano, jina *Selemani* hutamkwa kwa kuvuta silabi ya kwanza na kutumia nguvu katika utamkaji wa maneo hayo na kuwa ‘*Seele.*’ Utamkaji huu ni wa kawaida katika ufupishaji wa majina kwa jamii ya Wasukuma. Kwa hiyo, kutokana na mifano hapo juu, ni dhahiri kuwa hata majina ya kigeni

yanapotumika miongoni mwa Wasukuma huweza kufupishwa hasa katika lugha ya mazungumzo.

3.2.2 Kufupisha Mwanzoni mwa Jina

Hili ni kundi lingine la ufupishaji wa majina ya watu yenye asili ya kigeni. Ufupishaji huu unahusisha uondoaji wa viambishi mwanzoni mwa jina la kigeni. Majina ya kigeni huweza kufupishwa na kuingizwa katika kundi hili kwa kuwa ufupishaji wake huondoa viambishi mwanzoni mwa jina. Utafiti huu umechunguza majina kadhaa ya kigeni na kuona namna ambavyo hufupishwa na wazungumzaji wa lugha ya Kisukuma. Mifano yake ni kama ifuatavyo:

Mfano 6

Na.	**Jina kamili**	**Jina lililofupishwa**	**Viambishi vilivyoondolewa**
i	Anthony	Nton	‘A’
ii	Winifrida	Frida	‘Win’
iii	Christina	Tina	‘Chris’
iv	Angelo	Njelo	‘A’
v	Fredrick	Riki	‘Fred’
vi	Abdulazizi	Azizi	‘Abudul’
vii	Abdulykarimu	Karimu	‘Abdully’
viii	Maimuna	Muna	‘Mai’
ix	Innocencia	Cencia	‘Inno’
x	Santina	Tina	‘San’

Chanzo: Data za Utafiti (2025)

Ufupishaji huu wa majina unahusisha uondoaji viambishi mwanzoni mwa jina. Kwa mfano, jina *Abdullykarimu* limefupishwa na kuwa *Karimu* na *Christina* kuwa *Tina*. Kwa hiyo, utafiti huu umebaini kuwa ufupishaji wa kuondoa viambishi mwanzoni mwa jina hufanya jina kuwa fupi kulingana na matakwa ya wazungumzaji. Kwa mintarafu ya ufupishaji wa majina hayo, Bauer (1983) anabainisha kuwa hakuna njia mahususi ya kujua kuwa ni maneno mangapi hukatwa wakati wa ufupishaji kwa kuwa ufupishaji unaweza kufanyika kwenye sehemu yoyote ya neno.

3.2.3 Ufupishajii wa Jina Katikati ya Jina

Utafiti huu ulibaini kuwapo kwa ukataji wa kuondoa baadhi ya silabi katikati ya jina. Majina ya kigeni yamechunguzwa na kubainika kuwa ukataji huu pia upo kwenye kundi hili. Ifuatayo ni mifano ya majina ya kigeni ambayo hufupishwa katikati ya jina:

Mfano 7

Na	Jina kamili	Jina lililofupishwa	Viambishi vyoondolewa
i	Augustine	Gusi	'Au na 'tine'
ii	Elizerbeth	Zabe	'Eli'
iii	Abdulahimu	Dula	'Ab' na 'himu'
iv	Stanslaus	Lau	'Stans' na 's'

Chanzo: Data za Utafiti (2025)

Majina haya yanaonesha kuwa ufupishaji wa majina ya kigeni hufupishwa hata katikati ya jina, kwa mfano, jina *Stanslaus* hufupishwa na kuwa *Lau* na *Augustine* kuwa *Gusi.* Ufupishaji huu hauzingatii kanuni ya aina yoyote. Jambo kuu linalozingatiwa na watumiaji wa lugha hii ni kufupisha jina ambalo litakuwa rahisi kwao kuita au kuzungumza kama ambavyo tumeona katika aina zingine za ufupishaji. Utafiti huu umechunguza namna majina ya watu yanavyofupishwa miongoni mwa jamii ya Kisukuma wakati wa mawsiliano ya kila siku.

3.2.4 Ufupishaji wa Majina Ambatani ya Kigeni

Ufupishaji wa majina ya kigeni kwa jamii ya Wasukuma hufanyika pia kwa kufupisha majina ambatani ya kigeni wanayopewa pindi wanapozaliwa. Ufupishaji huu hufanyika katika majina ya kigeni kama inavyooneshwa katika Mfano Na. 6 ufuatao:

Mfano 8

Na	Jina kamili	Jina lililofupishwa	Jina lililoondolewa
i	Mwanahamisi	Mwana	*'Hamisi'*
ii	Mwanahawa	Hawa	*'Mwana'*
iii	Annamaria	Anna	*'Maria'*
iv	Rosemary	Rose	*'Mary'*
v	Abdulnassir	Abdul	*'Nassir'*

Chanzo: Data za Utafiti (2025)

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa ufupishaji wa majina ambatani ya kigeni hufanywa kwa kuondoa jina mojawapo wakati wa utamkaji na kufanya jina kuwa moja. Katika Mfano 6 hapo juu, majina yaliyotolewa hapo juu yanadhihirisha kuwa ufupishaji wa majina ambatani ni uondoaji wa jina mojawapo kati ya yale yaliyoambatishwa. Ufupishaji huu unaweza kufanywa kwa kuondoa viambishi vyote vya jina la mwanzo au jina la pili kutegemeana na matakwa ya wafupishaji wa jina hilo. Mfano jina *Annastella* linaweza kufupishwa mwanzo au mwishoni na kuwa *Anna* au *Stella*, *Abdulazizi* kuwa *Abdul* au *Azi*zi, *Resomary* kuwa *Rose* au *Mary*. Bauer (1983) anaeleza kuwa hakuna kanuni mahususi au seti ya sheria inayoweza kuatabiri ni sehemu gani ya neno itafutwa wakati wa ufupishaji ambao

hutegemea zaidi matumizi na mazoea ya jamii ya husika. Kwa hiyo, ufupishaji wa majina ya watu hutegemeana na matumizi ya jamii, urefu wa sauti na utambulisho wa jamii husika. Hivyo, hakuna sheria inayaoongoza ufupishaji wa majina ya watu.

4.0 Hitimisho la utafiti

Utafiti huu uliangazia uchamabuzi wa ufupishaji wa majina ya watu wanayopewa Wasukuma wanapozaliwa. Ufupishaji huu ni maarufu sana kwa kuwa hurahisisha mazugumzo yao ambayo kwa kiasi kikubwa hutawaliwa na ufupishaji katika kuitana majina. Data zilizochambuliwa zinadhihirisha kuwa majina ya watu hufupishwa mwanzoni, katikati na mwishoni mwa jina. Pia, utafiti huu umebaini kuwa majina ambatani ya Kisukuma na majina ya kigeni hufupishwa na kubaki jina mojawapo kati ya majina hayo kwa kuwa viambishi vya jina mojawapo huondolewa vyote na kubaki viambishi vya jina moja. Katika ufupishaji wa majina ambatani, watafiti wamebaini kuwa mzungumzaji hufupisha jina hilo kwa kutumia jina mojawapo, ambapo linaweza kuwa jina la kwanza au jina la pili ambalo ni rahisi kulitamka wakati wa mazungumzo.

Marejeleo

Adams, V. (1973). *An Introduction to Modern English Word-Formation*. London: Longman.

Bauer, L. (1983). *English Word- Formation*. Cambridge: Cambridge University Press.

Cohen, L. (2007). *Research Methods in Education* (6th ed.). London: Routledge Falmer.

Cohen, L., Manion, L., na Morrison, K. (2000). *Research Methods in Education* (5th ed.). London: Routledge Falmer.

Crystal, D. (1987). *The Cambridge Encyclopedia of Language.* Cambridge: Cambridge University Press.

Cozyb, P.C. na Bates, S.C. (2012). *Method in Behavioral Science Research*. New York McGrwa-Hill Press.

Fairclough, N. (1989). *Language and Power*. New York: Longman.

Fandrych, I. (2004). *Non-morphometric Word-formation Processes: A Multi-level Approach to Acronyms, Blends, Clippings and Onomatopoeia*. Bloemfontein: University of Free State.

Jang, H. (2023). "Monosyllabic Affective Hypocoristics of Korean Names." *Formation and Segmental Alternation*. 41: 87-110

Lopez-Rúa, P. (2002). "On the structure of Acronyms and Neighbouring Categories". *English Language and Linguistics* 6(1): 31-60.

Marchand, H. 1969. *The Categories and Types of Present-day English Word-formation*. Munich: C.H. Beck'sche Verlagsbuchshandlung.

Massamba, D.P.B. (2004) *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D.P.B. (2006). “Kiswahili cha Musoma, Mwanzo wa Lahaja Nyingine?” *Kiswahili.* 69: 37-51.

Mattiello, E. 2013. *Extra-grammatical Morphology in English: Abbreviations, Blends, Reduplicative and Related Phenomena*. Hawthorne: Walter de Gruyter.

Mekacha R. D. K. (2011). *Isimujamii. Nadharia na Muktadha wa Kiswahili* Dar es Salaam: TUKI

Msanjila, Y.P., Kihore, Y.M. na Massamba, D.P.B. (2009). *Isimujamii Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.

Mutembei, A.K. (2009). *Ukimwi katika Fasihi ya Kiswahili 1982-2009*. Dar es Salaam: TUKI.

Muzare, J. (2000). *African personal Names, The Great Lakes Areas*. Lantham MD: Scare Crow Press.

Newman, P. na Ahmad, M. (1992). “Hypocoristic Names in Hausa”. *Anthropological Linguistics.* 34 (1/4): 159-172.

Otlogetswe, T. J na Ramaeba, G. N. (2022). “Nickname Creation through Shortening Setswana Personal Names”. *South African Journal of African Languages*, 42(2): 200-206.

Pérez-Hernández, L. (2024). “Hypocorisms Meet Sound Symbolism: A Socio-Onomastic Study of Spanish Hypocoristic Forms of Personal Names in -”". *Voprosy Onomastiki*, 21(1): 72-95.

Plag, I. (2003). *Word-Formation in English*. Cambridge: Cambrige University Press.

Rico-Sulayes, A. (2020). The Use of Hypocorisms and Last Names as a Stand in for Proper Names: Distributional Differences between English and Spanish. *Lingvisticae Investigationes* 43(2), 317-337.

TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.

TUKI (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Toleo la 3). Nairobi: Oxford University Press.